# WITO WA MAOMBI YA RUZUKU KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA LUGHA YA ALAMA MAHUSUSI KWA ASASI ZA VIZIWI TANZANIA

Januari 15, 2019

## 1. UTANGULIZI

Foundation for Civil Society (FCS) ni asasi huru iliyoanzishwa kama taasisi ya kimaendeleo isiyozalisha faida, inayotoa ruzuku na huduma za kujenga uwezo kwa asasi za kiraia (AZAKI) nchini Tanzania. FCS ilisajiliwa na kutambulika rasmi kama chombo kilichopo kisheria mnamo Septemba ya 2002 na ikaanza shughuli zake rasmi mnamo Januari 2003.

FCS inafanya kazi katika kuhakikisha kwamba asasi za kiraia Tanzania zinakuwa chachu kwenye michakato ya maendeleo yenye kulenga kuleta mabadiliko kwa wananchi huku ikizingatia haki za makundi maalum katika jamii kama: Watu wenye Ulemavu, Wanawake, Watoto, Vijana na jamii zilizopo pembezoni.

Toka kuanzishwa kwake FCS imekua ikifanya kazi ya kuyajengea uwezo na kutoa ruzuku mbalimbali kwa mashirika ya Watu wenye Ulemavu ili kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanapata fursa mbalimbali sawa sawa na watu wasio na ulemavu katika jamii kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Watu wenye Ulemavu (2010) na Mkataba wa Kimataifa wa Watu wenye Ulemavu (UNCRPD) wa mwaka 2006.

Kwa mwaka 2019, FCS inatarajia kutoa ruzuku kwa mashirika yanayojishughulisha na utetezi wa haki za viziwi na vyama vya viziwi ili kuweza kutekeleza miradi ya kukuza na kuongeza uelewa wa Lugha ya Alama kwa Watumishi wa Jeshi la Polisi, Magereza na Mahakama. Lengo kuu likiwa ni kuhakikisha kuwa Viziwi wanapata haki zao katika vyombo hivi muhimu vya ulinzi, usalama na maamuzi.

## 2. WITO WA MAOMBI YA RUZUKU KWA AZAKI ZA VIZIWI

Sheria ya Watu wenye Ulemavu (2010) sambamba na masuala mengine inatoa fursa ya kupata taarifa, kulindwa na kushiriki au kushirikishwa katika masuala ya kawaida ya kijamii kwa Watu wenye Ulemavu sawa na watu wengine katika jamii. Aidha, sheria hiyo inabainisha umuhimu wa kutoa huduma za kijamii kwa uwazi na kuheshimu utu na uhuru wa kila mtu wakiwepo Watu wenye Ulemavu. Kwa mujibu wa sheria hiyo, vyombo vya umma vinatakiwa kuzingatia utoaji wa Huduma za Jamii kwa Watu wenye Ulemavu bila kuwabagua au kuwatenga.

Viziwi ni miongoni mwa makundi haya na wanayo haki ya kuchangamana na watu wengine na kushirikishwa kikamilifu katika shughuli za jamii. Tena, Viziwi wanayo haki ya kusikilizwa ipasavyo na kupata haki kutoka katika vyombo vya ulinzi na maamuzi hapa nchini.

Hata hivyo kumekuwa na changamoto mbalimbali zinazouia upatikanaji wa usawa katika jamii kwa watu wenye ulemavu.  Sababu kuu zikiwa ni mitazamo hasi kutoka kwa jamii kuhusu ulemavu na watu wenye ulemavu, kukosekana kwa miundombinu rafiki kwa Viziwi, kukosekana kwa wakalimani wenye ujuzi, uelewa duni wa Lugha ya Alama baina ya watendaji wa vyombo husika na Viziwi ambayo ni kiungo kikubwa cha mawasiliano baina ya Viziwi na watu wengine.

Kwa kubaini changamoto hizo, FCS inakaribisha maombi ya ruzuku  kutoka katika Asasi za Kiraia za Viziwi na Vyama vya Viziwi, ambazo hazifungamani na Vyama vya Siasa, na hazitengenezi faida kutoka mikoa yote Tanzania kushiriki katika utekelezaji wa shughuli zinazolenga kuimarisha upatikanaji wa haki kwa viziwi kutoka katika vyombo vya ulinzi, usalama na maamuzi yaani Jeshi la Polisi, Magereza na Mahakama.

FOUNDATION
for Civil Society

Maombi ya ruzuku yafike FCS kuanzia tarehe ya kutolewa tangazo hili hadi tarehe 15 Februari 2019. Tunaomba kuwataarifu kuwa asasi zinazodhamiria kuleta maombi yao zifanye hivyo mapema ndani ya kipindi tulichobainisha hapo juu.

## 3. MALENGO, MATOKEO TARAJIWA YA PROGRAMU HII.

3.1 Malengo makuu ya kutekeleza programu hii ni:

- Kuboresha mawasiliano kati ya Viziwi na watendaji katika Jeshi la Polisi, Magereza na Mahakama.
- Kuhakikisha kuwa vyombo vya ulinzi, usalama na maamuzi vinatenda haki kwa Viziwi.

3.2 Matokeo yanayotarajiwa

- Kuongezeka kwa kiwango cha utoaji haki kwa Viziwi nchini.
- Kuanzishwa kwa dawati maalumu la walemavu (wakalimani) katika Jeshi la Polisi, Magereza na Mahakama.

3.3 Shughuli zitakazofadhiliwa

- Shughuli zenye ubunifu na zenye kuonyesha kipekee namna makundi tajwa yatafikiwa ili kufanikisha malengo makuu ya wito huu.

## 4. Kiwango cha ruzuku na Muda wa utekelezaji

FCS itatoa kiwango kisichozidi shilingi milioni ishirini (20,000,000) kwa kila taasisi kwa ajili ya kutekeleza mradi wa miezi minane (8).

## 5. Vigezo vitakavyo zingatiwa katika kuidhinisha miradi

Kigezo kikuu kitakachozingatiwa katika kuidhinisha na kuuthibitisha mradi wowote ili kupata ruzuku kutoka FCS ni baada ya kujiridhisha kwamba shughuli za mradi husika zinadhihirisha pasipo shaka kuwa zitawanufaisha (moja kwa moja au kwa njia nyingine) walengwa wa maombi haya kama ilivyobainishwa katika Malengo Makuu ya wito huu.

Vigezo vingine mahsusi ambavyo vitazingatiwa katika uidhinishaji wa mradi ni;

a) Ni kwa jinsi gani shughuli zilizopangwa katika andiko la mradi zinaendana na malengo makuu ya programu kama ilivyoelezwa kwenye tangazo.

b) Ni kwa jinsi gani utekelezaji wa andiko mradi unaweza kupimika na kuchangia katika kupelekea ufanisi, uwazi, uwajibikaji, urahisishaji wa upatikanaji wa huduma na utendaji wa vyombo vya maamuzi na vyombo vya usalama.

c) Uwezo na ubunifu wa miradi yenye kuleta tija kwa gharama nafuu.

d) Nafasi ya jamii, kama vile, uwakilishwaji na ushirikishwaji, kiwango cha uhusishwaji wa jamii katika kuandaa, kuitambua na kutekeleza miradi inayowahusu.

e) Kwa jinsi gani mradi utaweza kuinufaisha jamii hadi katika ngazi ya chini kabisa kwa uthibitisho wa takwimu na ushahidi.

f) Uwepo wa nyaraka zote za muhimu zinazohitajika katika fomu ya maombi, zikiwemo fomu ya bao mantiki, mpango kazi, na bajeti, zinazopatikana kwenye tovuti ya Foundation.

**Kumbuka:** *Orodha ya mambo yote muhimu imeambatanishwa katika fomu mpya ya maombi.*

**5.0 Taasisi zinazoalikwa kuleta maombi**

Taasisi na Asasi za Watu wenye Ulemavu katika Asasi za Kiraia za viziwi na Vyama vya Viziwi tu na zenye vigezo vinavyohitajika, zinaweza kushiriki katika utekelezaji wa programu hii. Tafadhali jaza fomu inayopatikana katika tovuti ya FCS; www.thefoundation.or.tz

## 6. Taasisi ZISIZOLENGWA kupata ruzuku.

FCS itatoa ruzuku kwa Taasisi ambazo zimesajiliwa kufanya shughuli ambazo hazizalishi faida. Kama maelezo na ufafanuzi zaidi vitahitajika juu ya kigezo hiki, basi wasiliana na FCS kabla haujafanya maombi yako ya ruzuku.

### FCS haitatoa ruzuku kwa:

- Udhamini na ufadhili
- Miradi au shughuli zitakazo fanyika nje ya Tanzania
- Miradi au shughuli ambazo zimeshawahi kufanyika na kukamilika.
- Miradi ambayo imekwisha wezeshwa ruzuku na mashirika mengine.
- Kutumika kama Malipo ya ziada kwa wafanyakazi wanaolipwa na taasisi husika
- Kipato cha mtaji kwa taasisi ndogondogo za fedha
- Maombi toka kwa wataalamu wa ushauri au watunisha mifuko kwa niaba ya taasisi.
- Watu binafsi
- Vyama vya siasa
- Miradi ambayo inalenga kuinufaisha dini/dhehebu Fulani, kabila Fulani au kikundi Fulani chenye mlengo wa kikabila.
- Sekta binafsi (isipokuwa kama haipo kwa ajili ya manufaa ya kuzalisha faida)
- Taasisi zenye madeni
- Waendesha Semina, warsha, na mikutano tu, isipokuwa kama ni sehemu ya shughuli zilizounganishwa na tokeo mahususi.
- Gharama kubwa zisizo tarajiwa (dharura)
- Utoaji wa huduma za jamii
- Maombi ya mkakati wa ruzuku katika utekelezaji wa miradi ya UKIMWI

### Jinsi ya kutuma maombi

Katika wito huu, zipo njia mbili za kutuma maombi, moja ni kwa njia ya rejesta; mbili, kwa njia ya mkono. FCS haitapokea maombi yoyote yale yatakayotumwa kwa njia ya barua pepe au mtandao. ASASI inatakiwa kupakua fomu na viambatanisho vyake kutoka kwenye tovuti ya FCS http://www.thefoundation.or.tz. Tafadhali tumia fomu sahihi zitakazokuwepo kwenye tovuti na sio vinginevyo.

Maombi kamili ya Miradi yatatumwa kama nakala halisi (hard copy) yapelekwe kwa:

Mkurugenzi Mtendaji

The Foundation for Civil Society

7 Madai Crescent, Ada Estate Plot No. 154

P. O. Box 7192

Dar es Salaam

Simu ya Mezani +255 22 266 4890-2

Simu ya Mkononi: +255 754 005708

Tovuti: **www.thefoundation.or.tz**